SEHEMU YA NANE

KUTUNGA SHERIA-MASHARTI YA JUMLA

Ufafanuzi kuhusu Miswada

66.-(1) Muswada wa Serikali ni Muswada unaowasilishwa Bungeni na Waziri au na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Muswada wa Mbunge maana yake ni Muswada unaowasilishwa Bungeni na Mbunge yeyote ambaye si Waziri.

Utangazaji wa Miswada ya Serikali

67.-(1) Kila Muswada wa Serikali utatangazwa katika Gazeti la Serikali katika matoleo angalau mawili, kukiwa na kitambo kisichopungua siku saba kamili kati ya toleo la kwanza na la pili.

Tangazo la kwanza la Muswada wa Serikali litatolewa na kumfikia Katibu kukiwepo angalau siku ishirini na moja kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza, litakuwa linaonyesha Muswada mzima, pamoja na maelezo yaliyotiwa saini na Waziri yanayotaja madhumuni na sababu za Muswada huo.

(2) Muswada wa Serikali utahesabiwa kuwa umetangazwa mara ya pili endapo kutawekwa taarifa katika Gazeti la Serikali inayotaja jina la Muswada, nambari na tarehe ya Gazeti la Serikali ambapo Muswada ulitangazwa mara ya kwanza.

(3) Masharti ya Fasili ya (1) na ya (2) za Kanuni hii yaweza kuwekwa kando, na kutenguka bila hoja yoyote kutolewa, kama Waziri atawasilisha Bungeni Hati iliyotiwa saini na Rais, inayoeleza kuwa Muswada wa Serikali uliotajwa katika Hati hiyo ni wa dharura, hivyo

kwamba muda uliopo hauruhusu Serikali kuweza kutekeleza masharti ya Fasili ya (1) na ya (2) za Kanuni hii.

(4) Haitakuwa lazima kwa Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa taarifa ya Muswada wa Serikali ambao anakusudia kuwasilisha Bungeni iwapo Muswada huo umekwisha kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Utaratibu kuhusu Miswada ya Wabunge

68.-(1) Mbunge yeyote ambaye si Waziri aweza kuwasilisha Bungeni Muswada wa Mbunge.

(2) Taarifa ya kuwasilisha Muswada wa Mbunge itapelekwa kwa Katibu na taarifa hiyo itaeleza jina la Muswada unaopendekezwa, madhumuni na sababu zake.

(3) Baada ya taarifa kutolewa, Muswada utatangazwa Gazetini kama inavyotakiwa kwa Miswada ya Serikali kufuatana na masharti ya fasili ya (1) na ya (2) za Kanuni ya 67, na madhumuni na sababu yatatiwa saini na huyo Mbunge anayehusika.

Miswada kusomwa mara ya Kwanza

69.-(1) Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Muswada wowote, waweza, baada ya taarifa kutolewa, kuwasilishwa Bungeni katika wakati unaostahili kufuatana na Orodha ya Shughuli ili usomwe mara ya Kwanza. Katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada unaohusika, bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo. Hakutakuwa na mjadala wowote wakati wa Muswada wa sheria kusomwa mara ya kwanza, na hivyo itachukuliwa kuwa Muswada umekwisha kusomwa mara ya Kwanza, na papo hapo Spika aweza kupeleka Muswada huo kwenye Kamati inayohusika, na Kamati hiyo itaanza kuchunguza Muswada huo mapema iwezekanavyo. Isipokuwa kwamba kwa madhumuni ya kufanikisha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, Spika aweza kupeleka Muswada wowote kwenye Kamati inayohusika hata kama haujasomwa mara ya kwanza.

(2) Kamati iliyopelekewa Muswada kwa mujibu wa Kanuni hii yaweza, baada ya kupata idhini ya Spika, kumualika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati hiyo, kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wake wa Muswada unaohusika.

(3) Kamati iliyopelekewa Muswada haitakuwa na uwezo wa kufanya mabadiliko katika Muswada huo kwa mujibu wa Kanuni hii, lakini

yaweza kumuomba Waziri au Mbunge anayewajibika kuhusu Muswada huo kufanya mabadiliko katika Muswada wakati ukishafika Bungeni.

Miswada kusomwa Mara ya Pili

70.-(1) Baada ya Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa Muswada kumwarifu Spika, kwamba Kamati hiyo imemaliza kufikiria Muswada ambao ulipelekwa kwa Kamati yake kwa mujibu wa Kanuni ya 69, Spika ataagiza Muswada huo uwekwe katika Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Kusomwa mara ya pili.

(2) Mara baada ya Waziri au Mbunge mwenye Muswada kuwasilisha hoja ya Muswada Kusomwa mara ya pili, Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa Muswada huo au Mjumbe mwingine wa Kamati aliyeteuliwa kwa ajili hiyo, atatoa maoni ya Kamati yake kuhusu Muswada huo. Baada ya hapo, kama Muswada unaohusika ni Muswada wa Serikali, Msemaji wa Upinzani atapewa nafasi ya kutoa maoni ya upande wa Upinzani juu ya Muswada huo; na kama Muswada unaohusika siyo Muswada wa Serikali, msemaji wa Serikali atapewa nafasi hiyo ya kutoa maoni ya Serikali juu ya Muswada huo.

(3) Iwapo katika hatua hii, Waziri anataka kufanya mabadiliko katika Muswada huo kutokana ama na ombi lililofanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 70(6) au kwa sababu nyingine yoyote, basi atamjulisha Mwandishi Mkuu wa Sheria ili atayarishe, na Katibu atamgawia kila Mbunge, ama:-

(a) Nakala ya Muswada uliochapishwa upya, inayoonyesha wazi yale mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa; au

(b) Nakala ya orodha ya mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa. Endapo orodha ya mabadiliko hayo itatayarishwa, basi yaweza kuambatishwa kwenye Orodha ya Shughuli.

(4) Vile vile katika hatua hii, Mbunge yeyote aweza kuwasilisha kwa Katibu taarifa ya maandishi kuhusu mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima. Taarifa hiyo sharti ionyeshe bayana mabadiliko hayo yanayokusudiwa kufanywa katika Ibara gani ya Muswada; na masharti ya Kanuni ya 47 pia yatatumika kuhusiana na mabadiliko hayo. Nakala ya mabadiliko yoyote ambayo

yatakuwa yametimiza masharti ya fasili hii itaambatanishwa kwenye Orodha ya Shughuli.

(5) Hoja ya kutaka Muswada wa Serikali usomwe mara ya pili itakuwa hivi ifuatavyo:-

"Kwamba Muswada uitwao..... sasa usomwe mara ya pili au, kadri itakavyokuwa, "Kwamba Muswada uitwao..... kama ulivyobadilishwa kwa mujibu wa nakala mpya iliyochapishwa au kwa mujibu wa Orodha ya Mabadiliko iliyoambatanishwa kwenye Orodha ya Shughuli, sasa usomwe mara ya pili".

(6) Mjadala wakati wa Muswada wa Serikali kusomwa mara ya pili utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu. Lakini Mbunge yeyote aweza, wakati wa mjadala huo, kumuomba Waziri afanye mabadiliko katika Muswada, ama mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja Mbunge.

(7) Haitakuwa halali katika hatua hii kuleta hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja isipokuwa tu kwamba:-

(a) hoja yaweza kutolewa bila taarifa ya kubadilisha hoja "Kwamba Muswada huu sasa usomwe....." kwa madhumuni ya kuondoa neno "sasa" na kuongeza badala yake mwishoni mwa hoja hiyo maneno "baada.....muda atakaoutaja kuanzia leo".

(b) "mabadiliko yenye kutoa sababu" yanaweza kupendekezwa yafanywe katika hoja kwa kusema:- "Kwamba Bunge hili likatae Muswada huu kusomwa mara ya pili kwa sababu zifuatazo....." na hapo sababu za kupinga Muswada kusomwa zitatajwa kwa ukamilifu. Itabidi mtoa hoja ya kufanya mabadiliko ya namna hii atoe kwa Katibu taarifa ya hoja ya siku moja kabla ya kuitoa Bungeni.

Miswada kurudishwa kwenye Kamati

71.-(1) Endapo Muswada wa Serikali umesomwa mara ya pili na Waziri amemwomba Spika; wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima kupeleka tena Muswada katika Kamati inayohusika, basi Spika atafanya hivyo.

(2) Iwapo Muswada unapelekwa tena kwenye Kamati inayohusika, Mbunge yeyote ambaye wakati wa Muswada kusomwa mara ya pili alimwomba Waziri kufanya mabadiliko katika Muswada huo, na Mbunge yeyote ambaye, ametoa kwa Katibu taarifa kwa maandishi ya kutaka kufanya mabadiliko katika Muswada huo, aweza kuhudhuria mkutano wa Kamati hiyo na kushiriki katika mazungumzo akieleza mabadiliko anayopendekeza, lakini kama si Mjumbe wa Kamati hiyo hatakuwa na haki ya kupiga kura kuhusu uamuzi wowote wa Kamati hiyo.

(3) Kamati iliyorudishiwa Muswada kwa mujibu wa Kanuni hii itakutana mapema iwezekanavyo, kufikiria mabadiliko yaliyopendekezwa yafanywe.

(4) Kamati inayohusika haitakuwa na mamlaka ya kufanya mabadiliko katika Muswada uliopelekwa kwake kwa mujibu wa Kanuni hii, lakini yaweza:-

(a) Kumuomba Waziri afanye mabadiliko katika Muswada huo Bungeni;

(b) Kupitisha azimio la kutoa Bungeni taarifa maalum kuhusu Muswada huo.

(5) Baada ya Kamati kuwa imemaliza kuufikiria Muswada mara ya pili, Muswada utapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 72.

(6) Endapo Kamati iliyofikiria Muswada mara ya pili itaazimia kuwa taarifa maalumu juu ya Muswada huo itolewe Bungeni, Mwenyekiti wa Kamati atamwarifu hivyo Spika na taarifa hiyo itatolewa na Mwenyekiti au Mjumbe mwingine wa Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti, kabla Muswada huo haujawasilishwa katika Kamati ya Bunge Zima.

Miswada katika Kamati ya Bunge Zima

72.-(1) Bila kuathiri masharti ya Kanuni ya 71 endapo Muswada umesomwa mara ya pili, na majadiliano kuhusu ubora wa misingi ya Muswada huo yamekwisha, Bunge litaingia katika Kamati ya Bunge Zima. Lakini Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo, au Mbunge mwingine anayekusudia kuwasilisha mabadiliko katika Muswada huo kwa mujibu wa Kanuni ya 70(4); aweza kumwomba Spika kwamba hatua ya kuingia katika Kamati ya Bunge Zima iahirishwe hadi wakati atakaoutaja katika Ombi lake hilo, na Spika atatoa uamuzi wake kama atakavyoona inafaa.

(2) Isipokuwa kama Spika ataruhusu vinginevyo, muda wa kusema katika Kamati ya Bunge Zima utakuwa ni dakika zisizozidi tano. Waziri anayetoa maelezo ya Serikali hatawekewa muda, ili aweze kutoa majibu ya kuridhisha kuhusu hoja iliyotolewa.

(3) Kamati ya Bunge Zima itajadili na kupitisha, au kufanya mabadiliko na kupitisha Muswada Ibara moja baada ya Ibara nyingine, isipokuwa kwamba Mwenyekiti, akiona inafaa, aweza kuihoji Kamati itoe uamuzi wake kwa kundi moja lenye Ibara kadhaa au Ibara zote zilizomo katika sehemu moja ya Muswada.

(4) Mabadiliko yote yaliyopendekezwa na Waziri ili yafanywe katika Muswada wakati uliposomwa mara ya pili, pamoja na mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa kwa Waziri na Mjumbe yeyote wakati wa majadiliano ya hoja, yatajadiliwa na kupitishwa au kukataliwa au yatajadiliwa, yatabadilishwa na kupitishwa na Kamati ya Bunge Zima katika hatua hii kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi kwa ajili ya kushughulikia hoja.

Muswada Kusomwa Mara ya Tatu

73.-(1) Baada ya Kamati ya Bunge Zima kuwa imemaliza shughuli ya kufikiria Muswada kwa mujibu wa Kanuni ya 72, Waziri au Mbunge mwingine anayehusika na Muswada huo atatoa taarifa Bungeni kwamba "Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na kuukubali bila mabadiliko" au kama kuna mabadiliko yaliyofanywa, kwamba "Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na imeukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa" na papo hapo atatoa hoja ya kutaka Muswada huo usomwe mara ya tatu, kwa kutumia maneno yafuatayo:-
"Kwamba Muswada wa.....(Jina lake) sasa ukubaliwe" au, kama kuna mabadiliko yaliyofanywa katika Muswada, "Kwamba Muswada wa.....(Jina lake) kama ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe" na majadiliano juu ya hoja hiyo, kama yapo, yatahusu tu maneno yenyewe ya hoja.

(2) Hoja ya kupitisha Muswada wowote wa mabadiliko ya Katiba itaamuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 98 ya Katiba katika hatua ya Muswada huo kusomwa mara ya Tatu. Kwa sababu hiyo, kura zitapigwa kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.

Kuondoa Miswada

74. Waziri au Mbunge yeyote anayewasilisha Muswada aweza kuuondoa Muswada huo wakati wowote kabla ya Bunge kuhojiwa kutoa uamuzi wake, bila kuhitaji ruhusa ya Bunge.

75. Baada ya Muswada Kusomwa mara ya Tatu, Muswada huo utahesabiwa kuwa umepitishwa, na nakala za Muswada huo kama ulivyopitishwa zitatayarishwa, na Spika atapeleka nakala mojawapo kwa Rais mapema ili Rais atoe Kibali chake, au maagizo mengine atakayopenda kuyatoa. Kibali cha Rais kwa Miswada

76. Itakuwa ni wajibu wa Katibu kuwapatia Wabunge wote nakala ya kila Muswada uliotangazwa *Gazetini* kwa mujibu wa Kanuni ya 67. Kusamba za Miswada